# NGURUMO ya MWANDISHI

Toleo La V-Februari-MMXXII




**Tumefunika tena!**

Dawati la Mhariri:
0766-974 865

# TUMEFUNIKA TENA

**Mwezi wa pili ulikuwa wa furaha sana kwa waandishi wa Kitanzania. Tulishuhudia Tuzo ya Mabati-Cornel ikiendelea kudhihirisha kuwa waandishi wa fasihi ya Kiswahili kutoka Tanzania wanafanya vizuri katika tasnia hii.**

Kuna lipi la kuwaambia zaidi ya kongole nyingi kwao? Ushindi wao ni ushindi wetu sote, kwani maandishi yao yameitangaza Tanzania ndani na nje ya mipaka. Kiswahili kimekuwa lugha kubwa kwa sasa. Nchi nyingi duniani zinafundisha Kiswahili na hata kukitumia kwenye matangazo ya luninga na redio. Wenzetu wamekipa heshima, vipi sisi wenyewe tunaojiita Waswahili, tumechukua hatua gani kukiheshimisha?
Tunawashukuru sana Dr. Lizzy Attre na Dr. Mukoma wa Ngugi kwa ubunifu wao huu. Ubunifu wao ndiyo unaoibua vipaji vilivyojificha vya waandishi Watanzania. Tangu ianzishwe mwaka 2014 ushindani na mataifa jirani ulikuwa mkubwa lakini kwa sasa tuweze tu kusema kwamba Watanzania wameikamata.

Tukianza na Enock Maregesi ambaye kwa yeye naweza sema ndipo tuliifahamu tuzo hii, na wengine wengi walioipata kama Hussein Wamaywa, Zainab Baharoon, mshairi maarufu Bwana Doto Rangimoto. Tukamshuhudia na Lelo Mmasi, na mwaka huu Halfan Sudi na wengine wametung'arisha. Timu nzima ya Ngurumo ya Mwandishi tunakupongezeni sana, lakini tunawaomba jambo moja kwamba, tuzo mlizozipata ziwe chachu ya kuwaonesha njia na wengine ili dunia itambue kwamba ikitaka kuzipata riwaya bora za Kiswahili basi waje Tanzania. Hongereni na tunawatakia maisha mema.

## Mariam Mbano; Usimalize Kila Kitabu Ulichokianza…

**MWANDISHI ROBIN SHARMA katika kitabu chake cha WHO WILL CRY WHEN YOU DIE anasema kwamba DONT FINISH EVERY BOOK YOU START /USIMALIZE KILA KITABU UNACHOANZA SOMA.**
Watu wengi huwa tunaamini kwamba kila kitabu unachoanza kusoma lazima ufike mwisho wake au usome kwa kufuata mtiririko kwa maana uanze *page* ya kwanza hadi ya mwisho

Robin Sharma anasema kwamba sio kila kitabu unachosoma lazima umalize

Kuna vitabu unasoma kitabu kizima, kuna vile ambavyo unasoma baadhi ya *chapter* kuna vile ambavyo unasoma sehemu tu ya kitabu

Usione vibaya kwasababu umetumia pesa zako kununua kitabu au umehangaika kwa ajili ya kupata kitabu

Unaweza kusoma sura chache za kitabu teyari kimekuchosha, labda ulichotarajia kupata ndani ya kitabu hujakipata au kitabu kimekuwa kigumu kueleweka,unatumia muda mrefu kuelewa sehemu ndogo ya kitabu, umepoteza tu ari ya kuendelea kukisoma achana nacho sio lazima usome kila aina ya kitabu sio lazima umalize kila kitabu unachoanza kusoma

Kuna mtu alinambia yeye hawezi kusoma vitabu vyenye kuuana ndani yake kwa sababu huwa anayaona kama matukio ya kweli hivyo huwa vinamkosesha amani lakini anasoma na kuandika vitabu pia.

Ukiona unavutiwa na vitabu vya hadithi soma hivyo, vitabu vya siasa, historia au wasifu za watu pia soma ukipenda vya biashara au kujenga akili yako vyovyote unaweza kusoma

Mimi binafsi huwa simalizi kila kitabu nachosoma,kuna vitabu huwa nasoma naacha kabisa sitavisoma tena, kuna ambavyo nitasoma nitaacha nitarudi kukisoma tena, kuna ambavyo ili nimalize ni lazima nianze kusoma na vingine ili vinipe ari ya kuendelea kusoma hiko kitabu nilichoacha kuna waandishi wameliona hili na kulizungumzia kwa sababu kuna watu hata kitabu asielewe, kisimvutie mradi ameanza kukisoma basi lazima amalize

USIJITESE ACHANA NACHO/ NAVYO.

Kikubwa kumbuka sio kila kitabu unachoanza kusoma lazima umalize
***Marm***
***1/03/2019***

# TUZO YA MABATI: KIRUSI KIPYA YA HALFAN SUDI YAIBUKA KIDEDEA

**Tarehe 27 ya mwezi wa Januari mwaka huu, ilikuwa siku ya pekee ambayo ilibadilisha historia ya maisha ya Mwandishi Halfani Sudy na kumfanya kuwa mshindi namba moja wa Tuzo ya Mabati Cornell ya Fasihi ya Kiswahili.**

Hafla hiyo ya kutangazwa kwa washindi, ilifanyika katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa Lugha ya Kiswahili huku mgeni rasmi akiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa.

Jarida pepe la Sauti ya Ngurumo lilimfikia mshindi huyu aliyejinyakulia kitita cha Dolari za Kimarekani 5000 na kumhoji machache.

“Halfan Sudy, kwanza hongera sana kwa kutwaa tuzo ya Mabati Cornell ya Fasihi ya Kiswahili 2021. Umeiletea sifa Tanzania na umeipa heshima fasihi ya Kiswahili kwa Mara nyingine.

**Jibu:** Ahsante sana kwa kunipa hongera, ingawa hongera hii inatustahili waandishi wote duniani tunaoandika riwaya kwa lugha ya Kiswahili.

**Swali:** Unajisikiaje kwa kuwa mshindi wa Mabati 2021?

**Jibu:** Siwezi kuelezea kwa maneno kumaanisha ninavyojisikia, lakini ninajisikia vizuri sana kuliko wakati wowote ule katika maisha yangu kwa kuwa kushinda



tuzo ya Fasihi ya Afrika ya Mabati-Cornel. Heshima, ukubwa na thamani ya Tuzo ya Mabati-Cornell ndivyo vilivyonifanya nijisikie hivyo. Ilikuwa ndoto yangu kwa zaidi ya miaka sita, na ninashukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa ndoto hii imetimia.

**Swali:** Tuzo ya Kiswahili-ya Mabati-Cornell ya Fasihi ya Kiswahili ni nini? Unaweza kutuelezea kwa kifupi?

**Jibu:** Kwa kifupi, Tuzo ya Mabati-Cornell ni tuzo ya kazi za Fasihi ya Afrika iliyoanzishwa mwaka 2014 na Dr Lizzy Attre na Dr Mukoma wa Ngugi, lengo kuu la tuzo hii ni kuiinua Fasihi ya Afrika kwa kutoa tuzo kwa waandishi wa kazi za Fasihi kutoka Afrika na nchi zote zinazotumia lugha adhimu ya Kiswahili. Mabati-Cornell wanatoa fursa kwa waandishi kote duniani (*wa riwaya, ushairi na tamthilia*) kutuma kazi zao kwa ajili ya kuzishindanisha na hatimaye kutoa tuzo kwa kazi bora zaidi. Tuzo hii, sio tu inaiinua Fasihi ya Afrika, bali pia inasaidia kuikuza na kuiendeleza lugha yetu adhimu ya Kiswahili.

**Swali:** Kati ya riwaya zako ulizoandika, kwa nini au kitu gani kilikufanya uichague Kirusi Kipya kama karata yako ya ushindani?

**Jibu:** Kwa kifupi, hadi sasa nina vitabu vitano vya riwaya na miswada zaidi ya kumi. Sasa swali ni kwanini Kirusi Kipya? Kirusi Kipya ni riwaya bora zaidi kuwahi kuandikwa na mimi tangu nizaliwe. Riwaya bora kwa maana sahihi ya neno ‘bora’ linavyomaanisha. Fani katika Kirusi Kipya, maudhui ya Kirusi Kipya ndivyo vilivyonifanya niitumie kama silaha yangu ya ushindani. Na ninaweza kuthubutu kusema ilikuwa pia ni silaha yangu ya mwisho. Nikwambie tu, kuna kipindi wakati ninaiandika Kirusi Kipya, nilikuwa ninajisemea kimoyomoyo kwamba sidhani kama nitaweza kuandika tena kama nilivyoandika katika Kirusi Kipya.

***Inaendelea uk. Wa 7***

Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Faida za kusoma vitabu:


- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

# AMATA RIC kuirudisha JAMVI LA SIMULIZI App' HEWANI

MWANDISHI wa riwaya za kijasusi na muasisi wa Jukwaa la Jamvi la Simulizi Ndg. Richard Mwambe, anatarajia kuirudisha hewani *Appilication* yake ya Jamvi laSimulizi.

Akizungumza na jarida hili, Meneja wa mwandishi huyo Bi. Rehema Stanley ametuhakikishia kwamba *App* hiyo itapatikana kwenye simu za mkononi zinazotumia mfumo wa Android katikati ya mwezi March.

Bi. Rehema aliongeza kusema kuwa, wameamua kusogeza huduma za vitabu vya riwaya kwa njia ya nakala laini kwa kila mdau wa Kiswahili duniani. Kwa kuwa kwa mfumo huo wapenda riwaya popote walipo wataburudika, la muhimu tu ni kuwa na simu janja inayotumia mfumo huo.



**Bi. Rehema Stanley**

Pia ameeleza kwamba kwa kuweka *App* hiyo si kwamba hakutakuwa na nakala ngumu madukani, bali hii itasaidia kwa wasiopenda kubeba vitabu au kuhifadhi kwenye makabati yao. Aidha amewataka waandishi wabadilike kadiri ya teknolojia ya ulimwengu inavyobadilika kwani katika tafiti walioifanya hivi karibuni, Bi. Rehema anasema kuwa wasomi wengi wa vitabu wameangukia zaidi kwenye nakala laini kuliko zile ngumu.

Ameeleza pia zaidi ya riwaya katika *App* hiyo kutakuwa na Makala mbalimbali za kijasusi, jarida pendwa la Ngurumo ya Mwandishi, habari picha na kadiri wanavyoendelea maboresho zaidi yatafanyika.

Amesisitiza watu kuwa tayari kuipokea katikati ya mwezi Machi kama watakavyotangaziwa katika mitandao ya kijamii. Pia ametuhakikishia kuwa riwaya zote za Kamanda Amata TSA 1 zitapatikana bure na nyinghine kwa bei nafuu kabisa.

# Je; kusoma ni muhimu katika maisha yetu? - 5



**Na Mwandishi wetu**

**Katika toleo lililopita, tuliishia faida ya nne. Hapa basi tunaendelea na faida nyingine za usomaji vitabu.**

5. Huboresha uwezo wa kukumbuka


Unaposoma kitabu, utakumbuka mambo mengi kuhusu wahusika, maisha yao, historia, shauku, sambamba na matukio na mbinu zao ambazo zinafuma au kuitengeneza njia yao kufikia mafanikio katika kila simulizi. Hayo huwa tunayakumbuka daima, lakini ubongo ni kitu cha kushangaza sana na unaweza kukumbuka hivi vitu pindi tu ukikutana na mazingira yanayofanana navyo.

Kisayansi, ipo hivi, kila kumbukumbu mpya unayoijenga hufanya njia mpya *(synapses)* kwenye mishipa ya fahamu na kuimarisha zile ambazo zipo, ambazo husaidia kuishtua kumbukumbu ya muda mfupi *(short-term memory)* sanjari na kutuliza mihemko. Mtu yeyote aliyesoma kitabu kizuri kwa makini hata iwe miaka kumi nyuma ukimuuliza atakusimulia kuhusu hicho, ama Simulizi yenyewe au wahusika wake. Endapo atakutana na kitabu kipya, chenye maudhui yanayofanana na kitabu fulani cha zamani, mtu huyu hukumbuka kirahisi sana, atakwambia "mwandishi huyu kaandika kama fulani".

Hivyo usomaji wa vitabu unaongeza nguvu ya ubongo katika kukumbuka. Ndiyo maana hata wanafunzi darasani husisitizwa kujisomea ili kwenye mtihani waweze kukumbuka. Nani aliyesoma shule ya msingi miaka ya 1980-1987 asiyekumbuka Kisa cha Manenge na Mandawa katika kitabu maarufu cha Juma na Roza? Au kitabu cha riwaya cha Machimbo ya Mfalme Suleiman? Nikitaja tu jina la kitabu, aliyesoma atakumbuka wahusika wote.

Kusoma vitabu, majarida na makala kutatuwezesha kuwa imara katika kumbukumbu yaani kuboresha uwezo wetu wa kukumbuka. Hivyo ukitaka kuwa mahiri kwenye nyanja hii soma vitabu, jenga tabia ya kujisomea.

***Itaendelea toleo lijalo***




Makala ya Kijasusi

## VIRGINIA HALL, MWANAMKE ASIYE NA UMUHIMU— 02

**Na Mwandishi wetu**

Wakati Vita ya Pili ya Dunia ilipolipuka na kundi la NAZI la Ujerumani kuivamia Ufaransa, mwanamama Hall alijitolea kuendesha gari la wagonjwa la Wafaransa. Haukupita muda, Wafaransa wakamlazimisha kukimbilia Uingereza. Ilikuwa nafasi ya kukutana na ujasusi, hivyo wakamuunganisha na wanaintelijensia wa Kiingereza.



Baada ya mafunzo kidogo, huyu mwanamke Mmarekani mwenye mguu moja alikuwa miongoni mwa majasusi wa kwanza wa Uingereza kutumwa ndani ya NAZI iliyojikita huko Ufaransa mwaka 1941. Akajifanya mwanahabari wa gazeti la *New York Post*.

**Kufuatiliwa na Gestapo**

Kulikuwa na makosa, hasa katika siku za mwanzoni, wakati wenzake wa mtandao wake walipokamatwa na kuuawa.

Wajerumani wakagundua kwamba wapo mikononi mwa mwanamke mlemavu.
Lakini Hall alikuwa Jasusi wa kawaida, aliyepiga hatua moja mbele zaidi ya polisi wa siri wa Kijerumani, Gestapo.

"Virginia Hall, kwa upande fulani, alikuwa asiyependa," anasema Gralley. "Aliweza kuwachezea Gestapo anavyotaka. Hakuna hata mmoja wa Wajerumani katika vita ile aliyefikiri kuwa mwanamke huyo anaweza kuwa jasusi."

Hall alifanya kazi Ufaransa ya Mashariki huko Lyon. Na mara nyingi aliishi kwenye nyumba ya watawa wa kike na kuwashawishi wamsaidie.
Akajenga urafiki na mmiliki wa dangulo na kupata taarifa zilizohusu makahaba wa Kifaransa jinsi wanavyowalaghai vikosi vya Ujerumani.

Hall akawapanga wapiganaji wa Kifaransa, akawapatia nyumba salama na maswala ya kiintelijensia. Haya hayakufanyika bila kutambuliwa, anasema Purnell.

"Wajerumani waligundua kuwa wapo mikononi mwa mwanamke mlemavu," Purnell anaeleza.

Hall daima alikuwa akibadili mwonekano wake.

"Aliweza kuwa mwanamke wa aina nne tofauti kwa mchana mmoja, mwenye majina manne tofauti," Purnell anaendelea kusema.

Mwanaume mwenye harakati moto hakuwa mwingine zaidi ya yule mwenye sifa mbaya wa Gestapo, Klaus Barbie, aliyejulikana kama "Chinjachinja wa Lyon" maelfu wa Wafaransa waliteswa na kuuawa kwa mkono wake.
Barbie akatoa amri, "anatafutwa" tangazo kumhusu Hall lililoweka mchoro wa picha ya mwanamke huyo huku juu yake kukiwa na maandishi "Adui na jasusi hatari zaidi – lazima tumpate na tumharibu!" NAZI walionekana kuhakikisha wanamtia nguvuni Hall kabla ya mwisho wa mwka 1942. Akatorokea Hispania, ilikuwa safari ya kutisha iliyojumuisha kutembea mwendo wa siku tatu maili 50 kwenye barafu kali juu ya milima iliyopigwa marufuku ya Pyerenees.

***Inaendelea Ukurasa wa 6***

# VIRGINIA HALL, MWANAMKE ASIYE NA UMUHIMU—02

*Inatoka Uk. Wa 5*

Wakati nakitafiti hiki kitabu, Gralley, mpigambio za Marathon, alijaribu kuiga japo sehemu ya safari hiyo na kujikuta akishindwa.

"Najaribu kufikiri utashi na uvumilivu aliyokuwa nao uliompelekea kufanya hii safari," alisema Gralley, "si katika siku nzuri, lakini kwenye kipindi cha baridi kali na mguu bandia ambao alikuwa akiuburuta."

Hall alipofika Hispania, alikamatwa kwa kuwa pasipoti yake haikuwa na mhuri wa kuingilia nchi hiyo. Aliachiwa huru baada ya miezi sita, na akarudi Uingereza.

Alikuwa mtu asiyetulia na kutaka kurudi Ufaransa. Waingereza walimkatalia, walihofu ni hatari sana kwake.

**Kurudi Ufaransa**

Ijapokuwa Wamarekani walikuwa wakiongeza huduma yao ya kijasusi, bado hawakuwa na ofisi ya huduma za kimkakati huko Ufaransa au OSS. Wamarekani walimhitaji Hall, NAZI nao walikuwa kila mahali, wakihakikisha wanaweka ugumu kwa mwanamke huyo kufanya lolote, anasema Purnell.



"Akapata msanii wa kupamba uso ili amfundishe jinsi ya kuchora makunyanzi kwenye sura yake," anaeleza Purnell kwenye kitabu chake. "Pia alipata daktari mzuri sana wa meno kutoka London, akayachonga meno yake ya Kimarekani na kuyafanya kuwa meupe kama ya muuza maziwa wa Kifaransa."

Safari ya pili ya Hall kule Ufaransa mwaka 1944 na 1945, ilikuwa ni ya manufaa zaidi kuliko hata ile ya kwanza. Aliwapa mbinu wapiganaji wa upinzani, kuvunja madaraja na kuhujumu treni. Waliviweka pamoja vijiji kabla majeshi ya muungano hayajaingia ndani ya Ufaransa.

Mtandao wa Hall ulijumuisha watu 1,500, akiwemo askari aliyechanganya uraia Mwamerika-Mfaransa ambaye baadae alikuja kuwa mumewe, Paul Goillot. Mpwawe Hall, Lorna Catling, ambaye ana miaka 89 (wakati kikiandikwa kitabu hiki) anayeishi Baltimore, aliomba kukutana na mama yake mkubwa mara baada ya vita.

"Alikuja nyumbani nilipokuwa na miaka 16, alikuwa amepauka na nywele nyeupe na nguo kama mwendawazimu," Catling anasema.



Na ni kipi Hall alisema kuhusu vita?

"Kamwe hakuzungumza kuhusu hilo," Catling aliongeza.

Uingereza na Ufaransa, zote zinautambua mchango wa Hall – kwa siri. Rais Harry Truman alitaka kumpa Hall heshima hadharani wakati wa sherehe pale White House. Hall alikataa, akasema anataka kubakia *undercover* (asiyejulikana).

William Donovan, chifu wa OSS, alimpatia nishani ya huduma maalum – alimfanya kuwa mwanamke raia wa kwanza kuipokea katika Vita ya Pili ya Dunia. Mama yake Hall alikuwa mtu pekee kutoka nje White House kuhudhuria sherehe hiyo.

***Usipitwe na sehemu ya mwisho toleo lijalo.***


# TUZO YA MABATI: KIRUSI KIPYA YA HALFAN SUDI YAIBUKA KIDEDEA

*Inatoka ukurasa wa 3*

Na hii ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kutuma mswada katika tuzo za Mabati-Cornell na pengine ingekuwa ndio mara ya mwisho kama riwaya ya Kirusi Kipya isingeibuka na tuzo.

**Swali:** Hebu tuelezee kwa kifupi safari yako ya uandishi mpaka sasa ulipofikia...

**Jibu:** Kwa kifupi nimeanza uandishi baada ya kumaliza masomo yangu ya shahada ya kwanza ya Ustawi wa Jamii, mwaka 2014, mwaka uleule ambao tuzo za Mabati-Cornell zilianzishwa. Kabla ya hapo nilikuwa msomaji mzuri wa kazi mbalimbali za fasihi hasa riwaya kutoka kwa waandishi mbalimbali nchini. Pengine huo usomaji mzuri ndio ulionifanya niwe mwandishi mzuri.




Nilianza kuandika katika mitandao ya kijamii hasa Facebook kwa mwaka mmoja kabla sijamudu kutoa kitabu changu cha kwanza cha Penzi Chungu. Kwa sasa angalau ninajiona nipo sehemu, ingawa bado sijafika kileleni ninapopaota kila siku. Kuwa na vitabu vitano vya riwaya, na viwili kati ya hivyo kuchapwa na kampuni kubwa ya uchapaji ya Oxford University Press, EA. Kushinda Tuzo ya Mabati-Cornell kwa mwaka 2021 kiukweli kumenifanya nijione angalau nipo robo ya safari yangu ya uandishi wa riwaya ambayo marehemu mama yangu (Amina Baruan, Mwenyezi Mungu amrehemu) alikuwa anaiona miaka kadhaa nyuma.

**Swali:** Tunajua kwamba Tanzania kuna waandishi wengi sana wa riwaya, je kwa tuzo hii uliyoipata inakupa nafasi gani kati yao?

**Jibu:** Ni kweli Tanzania ina waandishi wengi sana, na kiukweli sijioni popote pale kwao, ila ninajiona popote nikijiangalia mwenyewe. Siwezi kuthubutu kusema mimi ni bora kuliko wao, HAPANA. Kila mwandishi ni bora kwa namna yake anayoandika, na namna wasomaji wake walivyompokea. Nimesema ninajiona popote nikijiangalia mwenyewe kwakuwa ninaona nimepiga hatua kubwa sana katika uandishi wangu, kwa namna nilivyoanza kuandika mitandaoni mwaka 2014, mpaka sasa nilivyofikia kutoa vitabu na kushinda Tuzo kubwa ya Fasihi ya Afrika ya Mabati-Cornell.

**Swali:** Unawaambia nini waandishi wa riwaya za Kiswahili?

**Jibu:** Kama kuna mambo matatu ninayoweza kuwaambia waandishi wa riwaya ya Kiswahili, basi, kwanza tuandike, pili tusome kazi za wengine na tatu kabla ya kutoa vitabu vyetu tuhakikishe vimepitia kwa wahariri. Tuandike kwa maana ndio maana tukaitwa waandishi. Mwandishi ni kuandika. Tusome kwa maana ya lengo la kupata mawazo mapya na kuona wenzetu wanaandika vipi, kuwa mwandishi sio kujifungia katika Kisiwa cha peke yako. Mwisho, ni muhimu kuzipitisha kazi zetu kwa wahariri ili kuhakikisha tunapunguza au kuondoa makosa yanayoweza kujitokeza. Hadithi hata iwe nzuri vipi, hupungua ladha endapo itakuwa na makosa mengi.

Washindi wengine waliojinyakulia zawadi katika siku hiyo ni pamoja na Mohd Omar Juma na kazi yake Chemchem Jangwani, Mbwana Kidato na kazi yake Sinaubi, Lucas Lubango na Bweni la Wasichana wakati Hafidhi Kido akiibuka na Kanzu ya Ukubwa.

Tuzo hii iliyojizolea umaarufu sana miongoni mwa walumbi wa Kiswahili hufanyika kila mwaka na kuwataka waandishi wa fasihi ya Kiswahili duniani kote kushiriki.

Ngurumo ya Mwandishi tunawapongeza wote waliojinyakulia zawadi za tuzo hiyo. ***RRM***

# MPIGA MBIO — 05

**Macho yalimwona huyo kijana, moyo ukamchagua, lakini bado mdomo ulikuwa mzito kusema 'nakupenda'. Alikumbuka siku moja akiwa kwao, na ukubwa huohuo alienda kumtembelea rafikiye Siyawezi.**

**Endelea…**

Siyawezi Mara baada ya kuhitimu kidato cha nne alijiunga jeshini, kazi aliyoipenda. Ikunda akiwa anapokelewa getini na rafikiye huyo kikosi cha wanajeshi waliokuwa mazoezini jioni hiyo walipita mchakamchaka wakiimba… (wenyewe wakiita 'chenja')

KIONGOZI
"Siku ya kwanza alisemaje?"
WOTE
"Mama naumia!"
KIONGOZI
"Siku ya pili akasemaje?"
WOTE
"Kidogo kidogo inaingia!"
KIONGOZI
"Siku ya tatu akasemaje?"
WOTE
"Leo utamu nausikia!"
KIONGOZI
"Siku ya nne akasemaje?"
WOTE
"Lini tena tutarudia?"

Wanajeshi wale waliimba wimbo huo kwa bashasha huku wakipiga mbinja kali za furaha, wakiwa wamevaa nguo zao za kivita zile za mabakamabaka na bunduki kubwakubwa mkononi huku kichwani juu ya ile kofia ya chuma, wamefunga majani.

Mmoja wao wakati wakipita hapo jirani akambania Jicho Ikunda huku akaendelea kuimba.

"Mxiuuuy…"

Ikunda akasonya. Sonyo lile likamfanya Siyawezi ageuke, "vipi! Mbona kusonya?"

……………

Simu ya Kenneth ilipokea arafa, alipoinyanyua na kuifuangua kikasha pokezi, moyo wake ukapiga pah! Hakuamini.

***'Imethibitishwa, akaunti yako imeongezwa Tsh 13,600,000…'***

"Shiiit!" akajikuta aking'aka peke yake. Ujumbe ule wa simu ulikuwa kama umempa nguvu mpya kijana huyu. Akajiinua kutoka pale kitandani na kukiendea kioo kikubwa kilichopo ukutani. Akajitazama. Ndevu zilikuwa kubwa kama za Morisson! Akavuta hatua mpaka kwenye kabati, akauvuta mlango na kuchukua shati lake la drafti, akalivaa. Suruali ya kadeti ya khaki na raba za Reebok. Akachukua waleti na kuifungua ndani. Haina kitu, zaidi ya kadi ya Benki ya Maendeleo ya Wazaramo. Akaifunga na kuitia mfukoni. Kenneth, akaiacha nyumba yake jioni hiyo na kuingia mjini. Alikuwa na uhakika wa pesa hivyo hakuwa na wasiwasi.

Breki ya kwanza ilikuwa Kariakoo karibu kabisa na mashine pesa ya ZDB (Zaramo Development Bank). Akatoa pesa takriban shilingi Milioni moja kwa mikupuo mitatu kama ambavyo mashine pesa ile ilivyomwelekeza. Akazisunda sehemu tofauti tofauti za mwili wake. Mara baada ya zoezi hill kukamilika akaondoka zake na kutafuta sehemu nzuri ili aweze kupanga mambo yake vizuri.
Samaki Samaki Restaurant, Mlimani City palimfaa. Aliketi kiti kilicho kwenye kona moja na kuacha kimoja ambacho kilikuwa maalum kwa mgeni atakayekuja. Akiwa katika tafakuri hiyo, simu take ikapata uhai, ikaita kwa fujo. Akainyakuwa na kuiweka sikioni. Alipoiruhusu iongee, alihisi mpigaji ana woga, anahema kupita kiasi.



Richard Mwambe

"Hello… naongea na Kenneth?" sauti ya kike iliyojawa kitetemeshi ililiza na kufuatiwa napumzi ndefu.

Riwaya ya MPIGA MBIO inatarajiwa kuwa katika mfumo wa kitabu. Weka oda yako sasa kupitia 0766974865

"Ndiyo! Nani mwenzangu?" akamjibu na kumtupia swali.
"Naitwa Ikunda, uliyeniachia mzigo pale benki…."
"Anhaaaa nimekukumbuka, nilikuwa nakuwaza sasa hivi!"
"Jamani, unaniwazia nini eti?" Ikunda akauliza huku akihisi kijinguvu kidogo kimemwingia.

***Itaendelea toleo lijalo***



**Na: Maundu Mwingizi**

**Kwa wasomaji wapya…**

**Mioyo yao huelemewa na haja zisizokubalika; masikio yao hutiwa uziwi na maombi ya haraka; na daima miili yao ni mawindo ya jeuri. Hunde akaenda kumposa Huria kwa mfalme Kisasi. Mfalme akamkatalia katakata.**


***Endelea***

Hunde akaudhika na kuanza kumbughudhi Huria mpaka wakapigana na mfalme Kisasi. Aliposhindwa akakimbia na kujiapiza kumkomesha Huria na kumwonesha kuwa yeye ni mwamba.

Basi ikawa kila alipopita Huria, Hunde alifanyiza jitihada mpaka akapagundua. Kila alivyojigeuza, naye alijigeuza vilevile na kuwa kama Mbwa anayenusa mtara wa windo. Alipojigeuza Panya, yeye alikuwa Paka; alipojifanya Paka, yeye alijigeuza Chui; na alipokuwa Chui, yeye akawa Simba; na hatimaye siku ile alipojigeuza Tandu, ndipo yeye akaibuka kama nyoka na kumkamata. Sheikh Shaaban Robert anasema: wanaume wana inda mbaya sana ufisadi unapowafusha. Kwa bahati tu, kabla Hunde hajamhasiri Huria ndipo Adili alipotokea na kumuua kwa kumponda na jiwe kichwani.

Malkia Mjeledi, alimshukuru sana Adili, akimwambia kuwa wema wake haukuoza. Kwa uwokovu aliomtendea Huria, maana yake aliwatendea wao wazazi wake fadhili na heshima kubwa mbele ya majini. Na kwamba sasa, ilikuwa zamu yao kumkirimu walivyoweza. Tazama: majini wanataka kukulipa wema...hapo ningelikuwa mimi Maundu mwana wa Mwingizi na pupa zangu, pengine ningetaka nilipwe magunia kwa maguni ya mali, kwa msaada kiduchu nilioutoa japo nikijua fika kwamba, wala sikutaraji kama kwa kumuua nyoka yule nilikuwa namsaidia binti mfalme wa ujinini. Lakini kama ambavyo jina lake linasadifu tabia zake za uadilifu, Adili alitafakari kwa muda na kumwambia malkia: "Deni langu limekwishalipwa lote. Niliokoa maisha ya binti yako, naye ameokoa maisha yangu. Hapana deni tena kati yetu."

Adili anatufunza kuwa na ulimi wa hadhari na ubongo wa hekima, kwa kutafakari na kutamka yale yenye kipimo. Ni kweli Adili alimwokoa Huria alipokuwa Tandu, naye Huria amemwokoa Adili baada ya kutoswa majaini. Lakini wakutanapo waungwana, huwa ni raha tupu kwa




namna ambavyo kila mmoja anazichanga karata zake. Ingalikuwa wewe ndiye malkia Mjeledi, pengine ungemwacha Adili aondoke zake kwa hoja kwamba hakuna tena deni kati yetu. Lakini kwa busara ya hali ya juu, malkia alimjibu Adili: "Usiseme kikembe, mwanangu. Wema wako ulikuwa asilia, nawe ulitangulia kuutenda; wa binti yangu ulikuwa wa kuigiza, naye ameutenda nyuma. Asili na uigaji ni vitu mbalimbali. Havilinganiki wala havitalinganika milele." Amaa kweli wema ni ule utendwao mwanzo, yafuatayo hapo huwa ni kulipana tu ihsani. Ukijitolea msaada japo kidogo bila kutaraji malipo, basi kuna siku utapata malipo makubwa kipindi ukiwa katika lindi la matatizo. Ukiyatazama maneno ya Adili na malkia Mjeledi, unaweza kuona kwamba viumbe hawa walijaaliwa uungwana na akili kubwa yenye kuchakata mambo kwa kasi, lakini ukweli ni kwamba wale ni wahusika wa kubuni tu katika hadithi, hivyo aliyewabuni na kuwalisha maneno hayo ndiye muungwana mwenye hiyo akili kubwa. Naye si mwingine bali ni mwalimu wetu Shaaban Robert. Kwangu mimi, huyu ndiye mwandishi wangu bora wa nyakati zote.

Kisa hiki cha ADILI NA NDUGUZE kinakwenda mbali zaidi, ambapo msomaji ataona namna Adili atakavyorejeshwa jahazini, namna ambavyo Huria binti Kisasi atakavyowatenda ndugu zake Adili; Mwivu na Hasidi. Mpaka kufikia mwisho wa kitabu hiki ni burudani na elimu tosha. Kwa apendaye na akitafute kitabu hiki amjue Shaaban Robert ni nani. ***Mwisho.***

**Andiko hili limeandaliwa na Mwanabalagha Maundu Mwingizi, Mtu wa Tabora. Maundu ni mwandishi wa riwaya za Kiswahili, mtundu wa Lugha ya Kisahili mwenye uwezo mkubwa wa kuichezea atakavyo.**

**Tangazo**

**MADUKA NA WAKALA WA VITABU NCHINI**

1-KONA YA RIWAYA
Kinondoni Morrocco
Nyuma ya jengo la Airtel
mob: 0655428085

2-POSTA MPYA
Kwa George-
karibu na Askari Monument
mob:0755454152

3-MOROGORO
Bima Samaki Samaki
Mob:0748623743

4-ARUSHA
Nje ya duka la Kimahama
Mob: 0757690302

5- MBEYA
Duka la vitabu
FANANI na HADHIRA
Mob: 0746840840

6-IRINGA
LUTENGANO stationary
Miyomboni

©ngurumo ya mwandishi 2022

www.richardmwambe.com

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**S.L.P 1039**
**IRINGA—TANZANIA**

**Instagram: jamvi la simulizi**

**Email: jamvilasimulizi"gmail.com**

**Whatsapp: 0734550514**

**Mob: 0766974865**
**0672160016**

## MWANDISHI WETU: RICHARD MWAMBE 'Kuandika ni kuandika tena'

Nimezaliwa Dar es salaam katika hospitali ya Ocean Road. Miaka ile ya 70 mpaka 80, wajanja wote wa Dar es salaam tulizaliwa hapo.

Nimekulia na kupitisha maisha yangu katika kitongoji cha Ukonga, mita chache kabisa kutoka Chuo cha Maafisa wa Magereza.

Elimu ya msingi nimepata katika Shule ya Msingi Ukonga na baada ya hapo nikajiunga na Chuo cha Ufundi cha Dar es salaam (Dar Tech)

Nimeanza kuandika riwaya rasmi mwaka 2012 kwa kukirudia kisa nilichowahi kukiandika nikiwa darasa la tatu, Msitu wa Solondo.

Mwitikio wa watu walivyoipokeza riwaya hii ndiyo ulionipa moyo wa kusonga mbele. Lakini nilikuwa navutiwa sana na uandishi wa mtu mmoja anaitwa Dadi Mwawale. Marehemu baba yangu Mwl. Mwambe alikuwa msomaji mzuri wa vitabu na alikuwa na masanduku yaliyojaa vitabu na kitabu cha huyu Dadi kilikuwamo.

Baada ya kujiunda katika uandishi wa riwaya za kijasusi ndipo nikaona niwe na visa vyangu vinavyofuatana. Hapo nikaibuka na mfululizo wa simulizi za mpelelezi pendwa Kamanda Amata.

Naweza sema kuwa Kamanda Amata amejizolea umaarufu sana kuliko hata mimi mwenyewe kiasi kwamba namwonea wivu.

Mpaka sasa nimeshachapa vitabu vinne; TUFAA JEKUNDU 2015, CRONOC 7 2016, MPATANISHI 2018 na HARUFU YA KIFO 2020.

Ukiachana na vitabu hivyo, nina riwaya 25 nyingine zinazomhusu TSA1 ambazo hazijachapwa.

Napenda tu kuwaambia waandishi, tusikate tamaa kwani kuandika ni kuandika tena.

